# Tume ya Haki za Binadamu ya Australia

## Kufanyakazi kuwadia jamii ya Australia ambapo haki zote za binadamu zinaheshimiwa, zinalindwa na kukuzwa

## Sisi ni nani

Tume ya Haki za Binadamu ilianzishwa mnamo mwaka wa 1986 kwa kitendo cha Bunge la Muungano.

Sisi ni shirika linalojitegemea la kisheria na tunaripoti kwa Bunge la Muungano kupitia Mkuu wa sheria.

## Muundo wetu

Tume hii ni shirika la kichuo liinalojumlisha Rais na Makamishna watano. Nyadhifa hizo tano kwa sasa zimeshikiliwa na watu watatu.

**Mheshimiwa Catherini Branson QC**
Rais na Kamishna wa Haki za Binadamu

**Bi. Elizabeth Broderick**
Kamishna wa Ubaguzi wa Kijinsia na Kamishna mwenye uwajibikaji wa Ubaguzi wa Umri

**Bw. Mick Gooda**
Kamishna wa Haki za Kijamii za wanainchi wa asili ya Australia na Wakazi wa Kisiwani cha Mlango Bahari i.

**Bw. Graeme Innes AM**
Kamishna wa Haki za Binadamu na

## Tunachofanya

Uwajibikaji wa Tume unajumuisha:

- elimu na uhamasishaji umma
- malalamiko ya ubaguzi na haki za binadamu
- kufuata haki za binadamu
- kukuza sera na sheria.

Tunafanya haya kupitia:

- kutatua malalamiko ya ubaguzi au ukeukaji wa haki za binadamu chini ya sheria za muungano.
- kufanya maulizo kwa umma kuhusu maswali muhimu kwa taifa, kama vile watoto wa kiasili kuondolewa kwa nguvu kwa familia zao na haki za watoto katika vituo vya uhamiaji.
- kuanzisha mipango ya elimu ya haki za binadamu na rasilimali kwa shule, kwa sehemu za kazi na jamii.
- kupeana ushauri wa kujitegemea ili kusaidia mahakama katika kesi ambazo zinahusisha kanuni za haki za binadamu
- kupeana ushauri na usaidizi kwa bunge na serikali ili kuanzisha sheria, mipango na sera
- kutekeleza na kupanga utafiti wa maswala ya haki za binadamu na ubaguzi.

## Utungaji sheria

Tume hii inauwajibikaji wa kuendesha sheria zifuatazo za muungano:

- *Sheria ya 2004 ya Ubaguzi wa Umri*
- *Sheria ya 1992 ya Ubaguzi wa Ulemavu*
- *Sheria ya 1975 ya Ubaguzi wa Kimbari*
- *Sheria ya 1984 ya Ubaguzi wa Kijinsia*
- *Sheria ya 1986 ya Tume ya Haki za Binadamu*

Tume hii pia inauwajibikaji maalum chini ya:

- *Sheria ya 1993 ya Jina la Kuzaliwa*, ili kuripoti kuhusu kazi hii na kufurahiwa kwa haki za binadamu za watu wa asili inayohusiana na jina la kuzaliwa (inayotekelezwa na Kamishna wa Haki za jamii za wanainchi wa asili ya Australia na Wakazi wa Kisiwani cha Mlango bahari)

- *Sheria ya 1996 ya Mahusiano Sehemu za kazi*, inayohusiana na matunzo ya muungano na malipo sawa (inayotekelezwa na Kamishna wa Ubaguzi wa Kijinsia).

## Malalamiko

*Sheria ya Ubaguzi wa Umri, Sheria ya Ubaguzi wa Ulemavu, Sheria ya Ubaguzi wa Kimbari* na *Sheria ya Ubaguzi wa Kijinsia* misingi yake yote ni mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu na mikutano iliyoidhinishwa na Australia. Sheria hizi zinawalinda watu dhidi ya ubaguzi au unyanyasaji katika maeneo ya kazi na pande kadhaa za maisha ya umma, msingi wake ukiwa umri, umbari, rangi, ukoo au taifa au asili ya kijamii, jinsia, ujauzito, hali ya ndoa au ulemavu.

Watu wanaweza kutoa malalamiko ya ubaguzi kwa Tume. Malalamiko huchunguzwa kwanza ili kuhakikisha yanaweza kuchunguzwa chini ya sheria ambazo Tume hii inauwajibikaji. Kisha malalamiko huhakikiwa ili kuamua kama yanapaswa kuondolewa au kama yanafaa upatanisho.

Upatanisho ni njia ambayo Tume huleta pande zote pamoja – mtu ambaye anatoa malalamiko na mtu au shiriki ambalo limelalamikiwa - ili kujaribu na kutatua swala hilo. Upatanisho ni njia ya faragha ambapo pande zote hupewa nafasi ya kuzungumzia maswala na kufikia makubaliano. Malalamiko mengi hufaulu kupatanishwa.

Kama malalamiko hayawezi kupatanishwa, yataondolewa na Rais. Kisha mwenye kulalamika anaweza kupeleka swala hilo kwa Mahakama ya Muungano wa Australia au Huduma ya Waamuzi wa Muungano ili waamue. Tume pia huchunguza malalamiko ya ubaguzi katika ajira na ukeukaji wa haki za binadamu chini ya *Sheria ya Tume ya haki ya Australia.*

Sheria hii hujumlisha:

- madai ya ukeukaji wa haki za binadamu na Jumuiya ya madola (kama vile idara ya serikali ya muungano) dhidi ya viwango vilivyokubalika vya kimataifa.
- ubaguzi katika ajira kwa misingi kadhaa, kama vile, dini, upendeleo wa ngono, maoni ya kisiasa, shughuli za chama cha wafanyakazi na rekodi ya uhalifu.

Malalamiko yaliyopokewa chini ya Sheria hii pia yanaweza kutatuliwa kwa upatanisho kati ya pande zote. Kama malalamiko hayawezi kupatanishwa, na hayajakomeshwa kwa sababu zingine zilizopeanwa katika sheria, basi Tume itapeana ripoti kwa Bunge la muungano likiorodhesha maswala muhimu na mapendekezo ya kutatua malalamiko. Malalamiko haya hayana haki zo zote za kisheria za lazima.

## Elimu na Ukuzaji

Mojawapo ya vitendo muhimu vya Tume ni kukuza uhamasishaji kuhusu Haki za binadamu nchini Australia – kuanzia kwa shule hadi kwa biashara na kwa kiwanda, kwa vikundi vya jamii hadi kwa serikali. Hii inajumuisha kukuza uhamasishaji wa haki za watu na uwajibikaji chini ya sheria za muungano za kupinga ubaguzi.

Ujumbe muhimu wa mipango yetu yote ya elimu ni kuwa kuchuja ubaguzi na unyanyasaji ni hatua muhimu ya kuhakikisha jamii vumilivu na yenye haki, ambapo Waustralia wote wanaweza kufurahiya haki zao.

Ili kufikia watu wengi kama iwezekanavyo, Tume:

- hufanyakazi na waalimu na wanafunzi, ili kukuza vipindi vya mtalaa-unganisho vya masomo kwa kutumia CD-ROM mkondoni na vifaa vya DVD
- hufanyakazi na wafanyakazi, ili kupeana habari na rasilimali ili kupunguza ubaguzi na unyanyasaji katika ajira
- hufanyakazi na vikundi vya jamii, ili kupeana habari na rasilimali ili kusaidiana kazi zao
- hufanyakazi na wanachama wa amali ya kisheria, kufanya semina na kuchapisha sasisha juu ya maswala ya kisheria za haki za binadamu
- hupanga mikutano na hafla, kama vile sherehe ya kila mwaka ya Medali na Tuzo za Haki za Binadamu.

Rais na Makamishna pia huhusika wakati wo wote ikiwezekana na vyombo vya habari, ili kukuza na kujadili maswala muhimu ya haki za binadamu na ubaguzi.

Tume ina tovuti ya kueleweka, ambayo ni rahisi kutumia, ambayo inajumuisha habari na rasilimali za watu, shule, wafanyakazi na vikundi vya jamii. Pia tuna uchaguzi mpana wa machapisho na.

Orodha ya barua za pepe, unaweza kujiunga ili kupokea maelezo ya hivi punde kuhusu shughuli za Tume.

## Maelezo ya mawasiliano

| | |
|---|---|
| **Anwani ya Mtaa:** | Level 8, Piccadilly Tower<br>133 Castlereagh Street<br>Sydney NSW 2000 |
| **Anwani ya Posta:** | GPO Box 5218<br>Sydney NSW 2001 |
| **Simu:** | (02) 9284 9600 au<br>1300 369 711 |
| **Faksi:** | (02) 9284 9611 |
| **TTY**: | 1800 620 241 |

**Tovuti:** www.humanrights.gov.au
Barua pepe:paffairs@humarights.gov.au

**Machapisho:** 1300 369 711 au
www.humarights.gov.au/about/publications

**Malalamiko:** 1300 656 419
Barua pepe ya malalamiko:
complaintsinfo@humanrights.gov.au

**Habari ya malalamiko mtandaoni:**
www.humanrights.gov.au/complaints_information

Maelezo katika lugha nyingine:
www.humanrights.gov.au/about/languages